# Chimbuko la Muziki wa *Hip hop* ni Uasi au Sanaa za Maonesho?

*E. Mahenge*

**Ikisiri**

Sanaa za maonesho ni utanzu wa kisanaa ambao unawakutanisha fanani na hadhira mahali pamoja kwa wakati mmoja – yaani wakati wa wasilisho la kisanaa. Muziki wa *Hip hop* ni aina ya muziki uliochipukia tangu miaka ya 1980 lakini ukapata mashiko kwenye miaka ya 2000 kutokana na ukuaji wa teknolojia ya kurekodia muziki. Muziki huu una mchanganyiko wa vionjo vya Kimagharibi pamoja na Kiafrika. Muziki wa *Hip hop* ni sanaa za maonesho kwa kuwa kuna uoneshwaji wa sanaa mbele ya watazamaji. Uoneshwaji huo ndio tunaouita sanaa za maonesho – yaani mwoneshaji na mwoneshwaji wanakuwepo katika tukio hilo kwa wakati huo. Makala inadadavua historia ya sanaa za maonesho pamoja na ile ya *Hip hop* na kuonesha ni kwa jinsi gani *Hip hop* ni sanaa za maonesho na sio uasi. Hoja hii imekuja kutokana na kauli ya Kwaku Person-Lynn (2001) anayedai kuwa *Hip hop* ilitokana na uasi wa vijana dhidi ya muziki wa dansi na disko uliokuwepo miaka ya 1970. Kazi ya makala haya itakuwa ni kuchunguza kama chimbuko la Hip hop ni uasi au sanaa za maonesho?

## 1.0 Utangulizi

Sanaa za maonesho ni utanzu wa kisanaa ambao unawakutanisha fanani na hadhira mahali pamoja kwa wakati mmoja – yaani wakati wa wasilisho la kisanaa. Muziki wa *Hip hop* (baadaye ukavuma kama Bongo Fleva au muziki wa kizazi kipya) ni aina ya muziki uliochipukia miaka ya 1980 lakini ukapata mashiko kwenye miaka ya 2000 kutokana na ukuaji wa teknolojia ya kurekodia muziki Tanzania. Muziki huu una mchanganyiko wa vionjo vya Kimagharibi pamoja na Kiafrika. Makala haya ni ya kidadisi yanayojaribu kuelezea historia ya sanaa za maonesho pamoja na ile ya *Hip hop* ili kuonesha ni kwa jinsi gani *Hip hop* ni sanaa za maonesho na sio uasi. Hoja hii imekuja kutokana na kauli ya Kwaku Person-Lynn (2001) anayedai kuwa *Hip hop* ilitokana na uasi wa vijana dhidi ya muziki wa dansi na disko uliovuma miaka ya 1970 huko Marekani. Lengo la makala haya ni kuchunguza kama chimbuko la *Hip hop* ni uasi au sanaa za maonesho katika muktadha wa Tanzania. Makala haya yana sehemu sita sehemu ya kwanza inahusu nadharia ya ushairi. Sehemu ya pili ni dhana ya sanaa za maonesho na historia yake nchini Tanzania. Sehemu ya tatu ni historia ya *Hip hop* na sifa zake pambanuzi. Sehemu ya nne inaelezea sababu za kutokukubalika kwa *Hip hop* nchini Tanzania katika miaka ya mwanzo. Sehemu ya tano inajadili ni kwa vipi *Hip hop* ni sanaa za maonesho au la, na mwisho ni hitimisho.

## 2.0 Ushairi ni Nini?

Dhana ya ushairi imefasiliwa na wataalamu mbalimbali, hatutaingia kwa kina katika jambo hili, bali tutapitia wataalamu wachache tu. Fasili za wataalamu hao tumezigawa katika mikabala miwili: wanamapokeo (wanaosisitiza urari wa vina na mizani) na wanausasa (hawasisitizi urari wa vina na mizani katika utunzi wa ushairi). Kwa mujibu wa Mnyampala (1965: vii):

> Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi.

Mnyampala anaendelea kusisitiza kipengele cha kutosheleza shida ama haja za shairi akitahadharisha wale wenye mtazamo kuwa shairi linapaswa liwe fupi na kwamba shairi refu ni baya – la hasha; kila shairi linapaswa lijitosheleze haja yake kama ni fupi au refu. Haipaswi kulazimisha shairi fupi liwe refu, na refu liwe fupi. Mtaalamu mwingine aliyezungumzia ushairi ni Shabaan Robert (1968:61), anasema:

> Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi, na tenzi zaidi ya kuwa sanaa ya vina ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhutasari. Mwauliza wimbo, shairi, na tenzi ni nini? Wimbo ni shairi dogo, shairi ni wimbo mkubwa, na utenzi ni upeo wa ushairi. Mwauliza tena kina na ufasaha huweza kuwa nini? Kina ni mlingano wa sauti na herufi. Kwa maneno mengine huitwa mizani ya sauti; na ufasaha ni uzuri wa lugha. Mawazo, maoni, na fikira za ndani zinapoelezwa kwa muhutasari wa ushairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.

Tatizo la fasili za Mnyampala (1965), na Robert (1968) ni kule kuona kwamba shairi linapaswa lipambanuliwe kwa vina na mizani. Wataalamu hawa wanaona kuwa vina na mizani ni uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili. Fasili zao zina dosari kwa kuwa, asili ya ushairi wa Kiswahili sio ushairi wenye urari wa vina na mizani. Asili ya ushairi wa Kiswahili ni nyimbo za kazi ambazo ziliimbwa sambamba na ufanyaji kazi pamoja na zile za kubembelezea watoto. Hebu tutazame mfano wa wimbo wa kubembelezea watoto:

> Silie mama silie
> Ukalia waniliza
> Wanikumbusha makiwa
> Makiwa ya baba na mama
> Wanioza dume kongwe
> Halisafiri halendi
> Kazi kumeza matonge (Mulokozi na Kahigi, 1978:12).

Dondoo hiyo inadhihirisha kuwa asili au chimbuko la ushairi wa Kiswahili halikutokana na nyimbo zenye urari wa vina na mizani. Kwa hiyo, dai la akina

Robert na Mnyampala halina mashiko. Kutokana na kukosekana kwa mashiko kwa hoja yao, hebu tuangalie maana ya ushairi kwa mujibu wa wanausasa, ambao waasisi wake katika ushairi wa Kiswahili ni Euphrase Kezilahabi, Ibrahim Hussein na Jared Angira. Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1982:25) ushairi ni:

> Sanaa iliyopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha, sitiari au ishara, katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo, ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kuelezea tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo (katika Mulokozi, 1996:96).

Fasili ya Mulokozi na Kahigi (1982) ndiyo tunayoikubali kuwa inajitosheleza katika kuelezea dhana ya ushairi. Fasili hiyo ina mawanda mapana kwa kuwa inaelezea ushairi kwa kuzingatia kanuni na misingi ya utanzu huu. Fasili yao inashadidiwa na Massamba (1983:60-94)) anapoelezea tanzu za ushairi wa Kiswahili kuwa ni pamoja na tumbuizi, nyimbo, shairi, tenzi, mashairi, na ngonjera. Massamba pia anagusia mitindo na miundo ya ushairi, na sifa za mtunzi wa ushairi kwamba anapaswa awe na kitu kinachomsukuma na sio kuwa na vina tu bila wazo. Vilevile ameongelea umuhimu wa mtunzi kuelewa falsafa za maisha za watu wengine na kuona anatofautianaje nao au anafanana nao vipi. Pia, mtunzi anapaswa kujua hisia za watu wengine kuhusu falsafa yake na wanapingana naye kwa vipi na kwa nini (Massamba, 1983:81).

Baada ya kuangalia maana za ushairi, ni vema kujiuliza ushairi wa *Hip hop* (Bongo Fleva au muziki wa kizazi kipya) unaangukia wapi? Je, ni *wanamapokeo* au *wanausasa?* Sasa tutadokeza kidogo kuhusu mgogoro wa ushairi wa Kiswahili ambao ulikuwepo katika jamii yetu tangu miaka ya 1970, 1980 hadi 1990, mgogoro ambao uliibua makundi mawili: wanamapokeo na wanausasa. Baadhi ya wanamapokeo ni pamoja na Amiri Sudi Andanenga, Mathias Mnyampala na Jumanne Mayoka kwa kuwataja kwa uchache. Kwa upande wa wanausasa, pamoja na waasisi tuliowataja hapo awali, ni Mugyabuso Mulokozi, Kulikoyela Kahigi, na Fikeni Senkoro, kwa kuwataja kwa uchache. Kama tulivyogusia hapo awali wanausasa walisimamia hoja kuwa, 'uti wa mgongo' wa ushairi wa Kiswahili sio vina wala mizani. Kinyume chake wanamapokeo waling'ang'ania msimamo kuwa 'uti wa mgongo' wa ushairi wa Kiswahili ni vina na mizani. Kwa mujibu wa Mulokozi katika muhadhara wa Ushairi wa Kiswahili alioufanya tarehe 21 Mei 2010 katika ukumbi wa ATB, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa wanafunzi wa shahada ya umahiri katika Kiswahili (MA Kiswahili) alieleza kuwa, wakati wa mgogoro huo kuna kijana alichapwa bakora. Kijana huyu alikuwa ni wa upande wa wanausasa na bakora hizo zilitokana na mabishano kuhusu *'Ushairi wa*

*Kiswahili ni upi?*' Mgogoro kama huu baina ya wataalamu unasaidia kujenga mjadala katika makala haya kuhusiana kama *Hip hop* ni uasi au sanaa za maonesho. Uasi pia ulionekana kwa washairi hawa wanaokiuka kanuni za vina na mizani.

**3.0 Sanaa za Maonesho ni Nini?**

Sanaa za maonesho ni tawi la sanaa za matendo ambazo huhusika na uoneshaji halisi wa tukio likiwakutanisha pamoja fanani na hadhira. Sanaa za matendo zinajumuisha matukio yanayotumia sehemu mbalimbali za viungo vya mwili kama vile uso, na kuwepo kwa fanani na hadhira kama njia ya mawasiliano. Mlama (2003) anaelezea kuwa sanaa za maonesho zinajumuisha sanaa ambazo huwasilisha wazo ana kwa ana kwa hadhira kwa kutumia usanii wa kiutendaji. Fanani na hadhira huwa pamoja. Mlama anabainisha vigezo vinne vinavyotumika kuipambanua sanaa ya maonesho. Vigezo hivi ni pamoja na dhana inayotendeka, mtendaji, uwanja wa kutendea, na hadhira. Naye (Mulokozi, 1996) anaainisha vigezo saba vya tamthiliya ambavyo ni watendaji, hadhira, ubunifu, kusudio la kisanaa, uwanja wa kutendea, muktadha wa kisanaa, na dhana inayotendeka. Tamthiliya ni sanaa za maonesho kwa kuwa ni sanaa inayowasilishwa mbele ya hadhira, ina utendaji, ina watendaji, na inahitaji uwanja wa kutendea. Pia, tamthiliya inakidhi vigezo sita vya sanaa za maonesho kwa mujibu wa Aristotle na Semzaba (1997) ambavyo ni maudhui, ploti, wahusika, muziki, uteuzi wa lugha na kionwa.

Kwa mujibu wa Mlama (2003:186) kuna aina kuu mbili za sanaa za maonesho. Aina hizi ni sanaa za maonesho za jadi na sanaa za maonesho za mamboleo. Sanaa za maonesho za jadi ni zile ambazo zimechimbuka kutoka katika jamii za Kitanzania. Sanaa hizo ni pamoja na ngoma, majigambo, miviga, jando na unyago, matambiko, utambaji wa hadithi na kadhalika. Katika shughuli hizi watu hufanya vitendo vya kisanaa kama vile uchezaji ngoma, uimbaji, upigaji muziki, utongoaji mashairi, vikiambatana na matendo ya mwili. Sanaa hizi zilisakamwa na wakoloni kwa kutumia mbinu ya elimu rasmi pamoja na dini ya Kikristo.

Sanaa za maonesho za mamboleo ni sanaa ambazo zinatokana na athari za ustaarabu wa kigeni. Hapa hasa tunaongelea drama ambayo ililetwa nchini na Waingereza wakati wa ukoloni. Kwanza wakoloni walileta drama ambazo ziliigizwa na Watanzania kama njia ya kujifurahisha, kwa mfano tamthiliya za Shakespeare ziliigizwa mashuleni ambako kulifanyika mashindano ya shule mbalimbali. Baadaye wanafunzi hawa walianza kutunga tamthiliya zao zilizohusu maisha katika jamii ya Tanzania. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yalistawisha sana vichekesho – aina mojawapo ya drama iliyoibuka kutokana na

drama ya Waingereza. Katika Tanzania ya leo, maonesho ya vichekesho ni mengi zaidi yakilinganishwa na drama (Semzaba, 1997).

Sanaa za maonesho zilikuwa na nafasi kubwa katika ustawi wa jamii kwa sababu ya kazi zake katika maisha na ustawi wa jamii hizo. Kwa mfano, sanaa zilitumika kama nyenzo muhimu kwenye dini, mawasiliano, matibabu, elimu, uhamasishaji, upatanishaji, uburudishaji na kadhalika (Lihamba 1985; Mlama 1991; Nyoni 1998 katika Makoye 2007). Kwa muhtasari, hiyo ndiyo maana ya sanaa za maonesho. Hebu tuangalie historia ya sanaa za maonesho nchini Tanzania.

**4.0 Historia ya Sanaa za Maonesho nchini Tanzania**

Historia ya sanaa za maonesho nchini inaweza kugawanywa katika vipindi vinne ambavyo Tanzania imevipitia katika historia yake. Vipindi hivyo ni kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, baada ya uhuru (wakati wa Azimio la Arusha), na mfumo wa vyama vingi vya kisiasa. Maelezo yake kwa ufupi ni kama ifuatavyo: Kabla ya ukoloni sanaa za maonesho zilikuwa chini ya uongozi wa wazee wa mila, waganga, watabiri, na viongozi wa koo (watemi). Hawa walikabidhiwa jukumu zito la kuitunza kutokana na umuhimu mkubwa uliokuwa ukitekelezwa na fani hii.

Wakati wa ukoloni ndipo sanaa ilianza kuingiliwa na tamaduni za nje kwa kuwa vijana waliokuwa katika mfumo wa kikoloni wa elimu walileteWa tamthiliya za Kiingereza ambazo walitakiwa kukariri na kuziigiza katika mashindano ya kishule yaliyokuwa yakifanywa wakati huo. Wakoloni walifanikiwa kuliteka kundi hili kwa kuwa lilikuwa bado halijaimarika katika itikadi ya jamii zao za Kiafrika. Kundi la vijana ni kundi ambalo linakabiliana na mambo kadha wa kadha kwa kuwa ni umri ambao bado haujajiimarisha katika kufahamu amali, tamaduni, na mila za jamii zao; jambo hili linawafanya vijana washawishike kirahisi na hivyo kufuata mkumbo.

Baada ya uhuru, yaani mwaka 1961 na kuendelea, kulikuwa na vichekesho ambavyo vilikuwa vikiigizwa bila kuandikwa - yalikuwa ni maigizo faraguzi yaliyokuwa yakikejeli wazungu weusi ambao sasa walikuwa wamekalia viti vilivyoachwa na wazungu halisi. Katika kipindi hiki ndipo Azimio la Arusha lilitangazwa mwaka 1967; lengo lake lilikuwa kutokomeza aina zote za unyonyaji kati ya mtu na mtu, na pia njia kuu za uchumi kuwa chini ya wakulima na wafanyakazi. Miaka michache baadaye kazi za kifasihi za kitashititi zilizokejeli Azimio hilo kutokana na upungufu wake zilijitokeza.

Awamu ya mwisho ni ile ya kuingia kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa, yaani kuanzia mwaka 1992 hadi leo. Katika awamu hii tunaona kuna uhuru wa kisiasa ambao unakwenda sambamba na uhuru wa vyombo vya habari na ndipo uhuru wa kisanii unapopata kazi zinazoongozwa na matakwa ya msanii bila kuijali hadhira yake. Hapa ndipo tunapokuta 'sanaa kwa ajili ya sanaa' ikiwa na maana kuwa, wasanii kwa kiasi kikubwa wanatunga kazi ambazo zinajisimamia zenyewe bila kuwa na uhusiano na jamii husika. Ni katika kipindi hiki ndipo muziki wa kizazi kipya unastawi kwa kasi na kuimarika.

**5.0 Muziki wa *Hip hop* au Bongo Fleva ni Nini?**

Historia ya muziki wa Bongo Fleva au kizazi kipya hapa Tanzania inaanzia katika muziki wa *Hip hop*. Inaeleza kuwa mnamo miaka ya 1980 na 1990 watoto wa Kitanzania kutoka familia zenye uwezo kiuchumi waliokuwa nje ya nchi kimasomo na kadhalika ndio walisaidia sana kuuleta muziki wa *Hip hop* au *rap*. Watoto hao waliporudi likizo nchini Tanzania walikuja na kanda, video na majarida ya muziki kuhusu wasanii wa *Hip hop* kutoka Marekani, Uingereza na nchi nyingine za ughaibuni. Vijana hawa walikuwa wakikutana kwenye fukwe mbalimbali, hasa Dar es Salaam, kujiburudisha na rafiki zao au vijana wengine kwa ujumla. Katika sherehe hizo madijei waliokuwa wakipiga muziki walimpa kinasasauti mtu yeyote aliyependa ku*rap*. Kwa namna hiyo muziki wa *Hip hop* ulikua na baadaye vijana wengi kujiunga. Ingawa muziki huo bado unaendelea lakini baadaye jina la Bongo Fleva lilishika kasi.

Elementi za muziki huu wa *Hip hop* ni pamoja na *graffiti, udijei, mabreka na uemsii*. Ufafanuzi wa elementi hizi kwa ufupi ni kwamba *graffiti* ni uchoraji wa maandishi ya wasanii kwa rangi za mafuta ambazo hazifutiki. Ilifanywa hivyo kama njia yao ya utambulisho kwa kuchora katika kuta au katika madaraja. *Udijei* ni mbinu ya kuchagua, kupiga miziki, kuchanganya na hata kuunda midundo mipya. *Mabreka* ni aina ya uchezaji ambapo mchezaji mmojammoja anajitokeza katikati na kuanza kucheza miondoko ya aina mbalimbali ikiwemo kujishika sehemu zake za mwili. *Uemsii*, kufokafoka au *rap* ni kipengele kimojawapo cha utamaduni wa *Hip hop* na ni aina ya ushairi, usimuliaji, au usemaji unaopangwa kivina kwa kufuata mdundo wa ala za muziki ambao ulisharekodiwa. Ni utamaduni ambao uliwakutanisha wale walionyimwa haki, walionyanyaswa, na kukandamizwa katika historia ukawa utambulisho miongoni mwa Wamarekani Weusi na Wakaribiani.

Wengi wa wasanii wa muziki wa kizazi kipya, yaani *Hip hop* na Bongo Fleva, hutumia majina mbalimbali ya kisanii. Kuhusiana na mavazi baadhi ya wasanii huchapisha na kuvaa fulana zenye majina yao au ya wanamuziki wanaowapenda. Wanawake huweza kuvaa nguo ambazo hazisitiri mwili kwa

kiasi kikubwa. Wasanii wengine hupendelea mitindo ya nywele kama vile kusuka na *dredi*, wengine hujitoga katika sehemu mbalimbali za miili. Halikadhalika, kwa baadhi ya wasanii matumizi ya bangi, *bifu* (ugomvi) au malumbano na matumizi ya misimu (maneno ya mtaani) ni baadhi ya sifa pambanuzi.

Ingawa wengine hutofautisha *Hip hop* na Bongo Fleva hata hivyo baadhi ya watu wanaona muziki wa Bongo Fleva hujumuisha aina mbalimbali za muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania. Baadhi yake ni *Hip hop* au *rap*; *rythym,* na *blues (R&B), dance hall, raga*; na *zouk*. Bongo Fleva inaweza kuchukuliwa kama tapo la kimuziki ambalo lilirekodi muziki kikompyuta na vifaa mbalimbali vya kielektroniki. Muziki huu ulitumia vionjo vya kiridhimu, mapigo, midundo na sauti kutoka nchi za Kimagharibi na Kiafrika. Muziki wa Bongo Fleva unachanganya vionjo mbalimbali vya Kimagharibi pamoja na baadhi ya vipengele vya kitamaduni, kimuziki, na kifasihi vya ndani na nje ya Tanzania ili kutengeneza muziki wenye upekee wa aina yake (taz. kwa mfano Perullo, 2003; Mangesho, 2003; Masonga, 2005; na Omari, 2009).

## 6.0 Kutokubalika kwa *Hip hop* Kulitokeaje?

Kutokubalika kwa muziki wa *Hip hop* hakukutokea Tanzania tu, bali pia sehemu mbalimbali duniani hazikuupokea muziki huu kwa mikono miwili. Jambo hili kwa hapa Tanzania tunaweza kulipatia ushahidi wake kupitia mazungumzo yaliyofanywa na mwandishi Hamis Dambaya na msanii mkongwe wa muziki wa Bongo Fleva, Joseph Mbilinyi maarufu kama Mr II au Sugu. Mazungumzo hayo yalifanyika katika kipindi cha *Keki ya Taifa* kilichoendeshwa na Redio Mlimani na Televisheni Mlimani siku ya Jumanne tarehe 31 Oktoba 2011. Mazungumzo hayo yaligusia suala la ***'uasi'*** ambao unajitokeza katika muziki wa *Hip hop*. Mr II alizungumzia kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika muziki wa kizazi kipya kutoka kwenye *'sanaa isiyokubalika'* mpaka kufikia hatua ya kukubalika. Mr II alikuwa anazungumzia jinsi *Hip hop* ilivyopokelewa na jamii ya Kitanzania wakati inaingia miaka ya 1990. Alisema "muziki huo haukukubalika lakini sasa unakubalika kwa kuwa ni muziki wa ukombozi".

Bwana Mbilinyi anaposema kuwa *'muziki huu haukukubalika'* alitolea ufafanuzi kuhusiana na utamaduni mzima wa *Hip hop*. Utamaduni huo unaonekana katika maisha ya wasanii wa hapa nyumbani. Utamaduni huu, kama tulivyogusia hapo awali, unahusisha mitindo ya mavazi ambayo yalionekana hayana adabu hasa kwa mabinti ambao walionekana wamevaa nusu uchi, tabia ya kusuka nywele na kutoga masikio kwa vijana wa kiume na matumizi ya lugha ya matusi katika baadhi ya nyimbo zao. Tabia nyingine ni matumizi ya lugha ya Kiingereza

(japokuwa kutumia Kiingereza si makosa inaweza kuchukuliwa kuwa ni mtindo wa msanii), pamoja na matumizi ya lugha ya mitaani, na uchezaji au unenguaji usio na maadili hasa kwa wasichana. Kwa ujumla mambo haya yaliwafanya watazamaji na wasikilizaji wa rika la utu uzima – yaani wazazi na wazee kutokuukubali muziki huu wa *Hip hop* kwa kuwa waliuhusisha na uhuni.

Hali hiyo ya utamaduni wa *Hip hop* ilijionesha pia katika video za nyimbo zao. Wimbo wa *Nalia kwa Furaha* (ingawa si miongoni mwa nyimbo za awali) ulioimbwa na Jackline Ntuyabaliwe maarufu kama K-Lynn akishirikiana na Maxmillan Bushoke ni mfano mzuri wa baadhi ya nyimbo ambazo hazikufurahiwa na baadhi ya watu. Katika video ya wimbo huu, K-Lynn anaonekana amevaa nguo za ndani na sidiria tu wakati anaingia kwenye bwawa la kuogelea. Isitoshe wakati anapanda kwenye pikipiki, amevaa sketi fupi sana ambayo anaipandisha zaidi ili isimzuie kukaa vizuri kwenye pikipiki. Si hivyo tu, Bushoke (ambaye ni kijana wa kiume) anaonekana ametoga masikio na amevaa hereni. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yaliwafanya Watanzania (hasa wazazi na wazee) wasiikubali sanaa hii wakati inaingia.

Jambo jingine lililopingwa na baadhi ya wasikilizaji na watazamaji wa Kitanzania wa nyimbo hizi za kizazi kipya ni 'ujigambaji'. Wasanii hawa walituhumiwa kwa kujisifia sana na kujigamba kwenye beti za nyimbo zao jambo lililowafanya baadhi ya watu wasiukubali ushairi huu. Ingawa inaonekana kujigamba kunakofanywa na wasanii wa muziki wa kizazi kipya kama ni 'uasi' hata hivyo inapasa hapa kusisitiza kuwa majigambo ni moja ya tanzu muhimu ya fasihi simulizi ya Tanzania na sehemu nyingi duniani (taz. pia Rubanza, 1994; Mulokozi, 1996; Omari, 2009; Samwel, 2012).

Tukirudi katika mahojiano ya Hamisi Dambaya na Mr II, kwa upande mwingine, Mr II anaelezea kuwa siku hizi nyimbo za *Hip hop* au Bongo Fleva zinakubalika. Kukubalika huku kunatokana na watazamaji na wasikilizaji wa nyimbo hizi kuona kuwa 'muziki huu sio uhuni' bali ni ajira. Mr II anasema, '*sasa unakubalika kwa kuwa ni muziki wa ukombozi*'. Wasanii wamekuwa mstari wa mbele katika kupinga umaskini, ufisadi, wizi, rushwa, na kutetea masuala mbalimbali ya kimaendeleo katika jamii kama vile haki za wanamuziki, watoto na walemavu. Hivyo basi ingawa awali muziki wa *Hip hop* haukukubalika kwa urahisi na wanajamii wasio vijana lakini baadaye muziki huu ulikubalika na kuonekana kuwa una mchango mkubwa katika jamii ya Kitanzania katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, siasa na uchumi.

### 7.0 *Hip hop* /Bongo Fleva ni Sanaa za Maonesho?

Ili kulijibu swali hili na kuweza kuonesha uhusiano uliopo hatuna budi kugusia dhana ya drama. 'Drama ni njia ya mawasiliano ya umma' (Masonga, 2005). Kauli ya Masonga inaweza kufafanuliwa kuwa drama ni namna inayowawezesha watu kuwasiliana kwa kutumia sanaa ya uigizaji. Uigizaji huu unajitokeza pia hata kwenye nyimbo za Bongo Fleva kutokana na kutumiwa kwa wahusika katika nyimbo hizo. Mathalani, kuna mhusika Binti Kiziwi katika wimbo wa msanii Ally Mohamed Ahmad maarufu kama Z. Anton uitwao ‘Binti Kiziwi’. Katika wimbo huu uhusika huu unawasilishwa na 'mwigizaji' ambaye ni binti mrembo anayeuvaa uhusika na kuigiza kuwa yeye ni kiziwi. Kwa hiyo, kauli ya Masonga ina ukweli fulani ndani yake kwa kuwa, kupitia udrama huo kuna mawasiliano kati ya wahusika/waigizaji wa wimbo huu na hadhira kwa kupata mawasiliano–kupitia lugha na vitendo. Masonga anaendelea kuelezea kuwa, hakuna fasili ya moja kwa moja ya drama - lakini ni ukweli usiopingika kuwa, kila jamii inatumia namna moja au nyingine ya drama katika maisha ya kila siku. Kitu cha msingi ni kwamba, kuna vielementi visivyobadilika katika drama ambavyo vinapatikana katika kila aina ya drama. Drama inaelezea hadithi zenye ukweli fulani katika maisha ya mwanadamu. Katika wimbo huo, drama inatufahamisha kuwa, kijana Z. Anton, ambaye ndiye mtunzi na mwimbaji wa wimbo huu amempenda binti ambaye ni kiziwi lakini anashindwa kuwasiliana naye ili amueleze hisia zake. Drama inatumia ubunifu; kwa kuangalia video ya wimbo huo, tunauona ubunifu wa mtunzi katika vipengele mbalimbali. Kwanza, anajaribu kutumia lugha ya alama pale anapounganisha vidole vyake na vya msichana ili kumwelezea kuwa anampenda. Anamchorea picha mbalimbali zinazoonesha au kuelezea hisia za mapenzi, anachora picha yake akionesha anadondokwa na machozi lakini binti kiziwi haelewi. Huo ni ubunifu na kuna mengi ambayo mtunzi ameyaonesha katika wimbo huo.

Drama inahusisha maisha ya kila siku ya jamii husika. Kwa mfano, katika jamii yetu tunao watu wenye mahitaji maalumu kama viziwi. Watu hawa wanahitaji kuwasiliana kama watu wengine wanavyofanya ingawa kuna ugumu wa kufanya mawasiliano kwa kuwa viziwi wana lugha yao ya alama ambayo baadhi ya wasio viziwi hawaijui. Jambo analoliwasilisha Z. Anton katika wimbo huu lipo katika maisha yetu. Ni muhimu kuzingatia kuwa hadhira ina uwezo wa kuhusisha drama na maisha ya kila siku.

Drama inabadilika kama ambavyo jamii inabadilika. Tushadidie kwa hoja ya Mr II kuwa hapo awali muziki wa kizazi kipya haukukubalika kirahisi lakini sasa umekubalika. Kwa hiyo kuna ukweli kuwa jamii inapobadilika na drama inabadilika. Si hivyo tu, hoja hii inajitokeza kwa Mlama (2003) anapoelezea

aina za sanaa za maonesho zilizomo katika jamii ya Kitanzania, kwamba kuna za jadi na zile za mamboleo.

Sanaa za maonesho za jadi na za mamboleo, hutumia waigizaji au wachezaji (watu) ambao hufanya matendo ya kisanaa mbele ya watazamaji. Waigizaji au watendaji hawa hutumia utu wao katika kuvaa uhusika mbalimbali. Kwa mfano, wimbo wa *Binti Kiziwi* unaelezea namna kijana alivyompenda msichana mrembo ambaye ni kiziwi. Binti Kiziwi ni mhusika tu ndani ya wimbo huu ambaye ameigiza kwa kijivika uhusika wa 'Binti Kiziwi'. Kwa hiyo, kipengele cha mhusika na uhusika (ambao hapa umevaliwa na mwigizaji) unajitokeza kupitia wimbo huo. Hebu tutazame mashairi ya wimbo huu wa *Binti Kiziwi*[1]:

**Ubeti wa 1**
Nimpate vipi mi sijui, nina imani mapenzi hayajui
Nitapata ugonjwa wa moyo, kwa sababu ya mawazo
Ninavyojua maisha yake, hajawahi kuwa na boyfriend
Ila ni mimi wa kwanza na ninashindwa kumpata
Kwa ishara inaonekana nampenda, yeye eti ninamzingua
Eti ingelikuwa anasikia, basi ukweli wangu angeujua
Kwa ishara inaonekana nampenda, yeye eti ninamzingua
Eti ingelikuwa anasikia, basi ukweli wangu angeujua
Ningelizoea rafiki yake basi yeye ningemtumaaaa
Ningezitambua ishara zake basi mi kwake ningefika

**Korasi**
Si siri ninampenda binti kiziwi
Moyo wangu ameuteka binti kiziwi
Si siri nateseka juu yake ye binti kiziwi
Si siri ninampenda binti kiziwi
Kwa kuwa moyo wangu ameuteka binti kiziwi
Kichwa kinauma mawazo kwake binti kiziwi

**Ubeti wa 2**
Nashangaa pale nampomkuta akiwa na wenzake wanaongea
Huwa najiuliza mimi wanaongea naye vipi
Nashangaa nnapomuita nahisi huwa anakataa
Sijui ndio hasikii, au mapozi, au mapozi naye
Afadhali angejua kusomae, hata chale kiumbe ningempa
Eti kama ningejua ishara, basi kwake ningefika mimi
Afadhali angejua kusomae, hata mbonge kiumbe ningempa
Eti kama ningejua ishara, basi kwake ningefika baby

**Rudia Korasi**
**Ubeti wa 3 (rap)**
Binti kiziwi yuko full yani yuko bomba

---

[1] Umepakuliwa kutoka http://www.museke.com/node/1211 tarehe 6, Novemba, 2011.

> Amenidatisha mnyamwezi na yake figure
> Tatizo moja tu ambalo mimi hulinasibu
> Kila kukicha hata nikiwaza mimi sipati jibu
> Nikimwambia neno I love you wala halijui
> Nikimwambie neno I need you halitambui
> Nikimwimbia nyimbo nzuri hata hasikii...

Tukiendelea kuchambua wimbo huu, tunaona sifa za 'muziki' ambayo imo ndani ya drama. Muziki unahusisha mipando na mishuko ya sauti za wazungumzaji na waimbaji. Kwa mujibu wa Masonga (2005), muziki ni elementi kubwa kabisa ya drama. Muziki pamoja na video za muziki zina nguvu kubwa katika kuelezea uzoefu wa wanajamii kwa kutumia taharuki. Migogoro inayoibuliwa katika nyimbo hizi inaelezea mambo yaliyomo katika jamii.

Hivyo basi, *Hip hop*/Bongo Fleva ina utajiri mkubwa sana wa elementi za kidrama. Muziki huu ni muhimu sana katika kuonesha mabadiliko yanayopaswa kutokea katika jamii zetu (Masonga, 2005). Onesho la kidrama (muziki wa Bongo Fleva) inaweza kuoneshwa jukwaani, kwenye televisheni, kwenye thieta, au chini ya mti. Kwa muktadha wa makala yetu, onesho hili la kisanaa ambalo ni wimbo wa *Binti Kiziwi* tumelitazama kupitia kwenye televisheni. Mwongozaji wa muziki huu wa Bongo Fleva anaweza kutaka waimbaji watumie muziki wa ala, wacheze, wazungumze, wafanye *maimu*, au mjumuiko wa yote hayo. Matendo hayo yanaweza kuwa yamefaraguliwa au yameandikwa. Katika wimbo wa *Binti Kiziwi* tunaona waimbaji (waigizaji) wanafanya *maimu*. Kwa mfano, msanii Z. Anton anawasiliana na Binti Kiziwi ili kumueleza hisia zake na anaimba. Yote haya yako ndani ya uamuzi wa mwongozaji wa muziki huu wa Bongo Fleva.

Kwa kuhitimisha sehemu hii tunasisitiza kuwa muziki wa Bongo Fleva hautenganishiki na sanaa za maonesho, kwani una uhusiano wa karibu sana na drama. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, kupitia wimbo wa *Binti Kiziwi*, elementi za kidrama zimejitokeza. Elementi hizi ni pamoja na hadithi zenye kuelezea ukweli fulani katika maisha, ubunifu, kubadilika kulingana na mabadiliko katika jamii, na uhusiano wa drama katika maisha ya kila siku ya jamii husika. Kwa kuzingatia mambo yaliyojadiliwa katika sehemu hii, muziki wa Hip hop/Bongo Fleva unazo sifa za sanaa za maonesho kama zilivyobainishwa na wataalamu kama Mulokozi (1996), Semzaba (1997) na Mlama (2003) kwamba zinazoonesha maisha kisanaa. Yaani ni kule kuyachukua maisha halisi ya mwanadamu na kuyaweka jukwaani.

Makala haya yanakubaliana na mawazo ya wataalamu wote watatu kuhusiana na sanaa za maonesho kwani ingawa wametumia maneno tofautitofauti lakini

dhana inayokusudiwa ni ileile. Hivyo, kulingana na maelezo yao, tunapata ushahidi kuwa *Hip hop* /Bongo Fleva imetokana na sanaa za maonesho zilizopo katika jamii ya Watanzania. Kutokana na utafiti wetu tumegundua kuwa aina zote mbili za sanaa za maonesho yaani za kijadi na zile za kimamboleo zinajitokeza katika muziki huu wa kizazi kipya au Bongo Fleva.

**8.0 Hitimisho**

Tuhitimishe makala haya kwa kupinga hoja ya Kwaku Person-Lynn (2001) inayodai kwamba, chimbuko la *Hip hop* au *rap* lilifungamana na itikadi za kuasi muziki wa disko ulioshamiri miaka ya 1970 nchini Marekani. Makala haya yanapinga dai hilo kutokana na ukweli kwamba hakukuwa na uasi wa aina yoyote ila uibukaji wa tapo hili ulitokana na watu weusi wa Marekani (Waafrika - Wamarekani) kutaka kujitambulisha baada ya kuona wanatengwa na kunyanyaswa (taz. Mangesho, 2003). Taratibu muziki huu ulizidi kusambaa na kuota mizizi katika nchi mbalimbali ulimwenguni. Hoja hii ya asili ya muziki wa *Hip hop* ambayo tunaipinga hapa, inaungwa mkono na Adrisa Banjoko ambaye anajiita 'The Bishop Of *Hip hop*'. Mchambuzi huyu na mwanaharakati wa muziki wa *Hip hop* aliandika makala inayoitwa *"A Response*: *Hip hop Is Indeed Black Culture"* ambayo alikuwa akipingana na hoja ya Kwaku kwenye kazi yake ya "*Rap Music: Afrika to Hip hop*". Kwaku anadai kuwa, *Hip hop* huko Marekani ilichipukia kutokana na 'uasi'. Adrisa anaelezea katika aya ya kwanza kuwa, 'kwa yeyote ambaye anasingizia kuwa, *Hip hop* haina asili ya Kiafrika na Kiafrika-Kimarekani kwa hakika anatukana na kuwafedhehesha sana watu wote ambao wanapenda sanaa hii...'

Hoja ya msingi ambayo ilikuwa inaongoza mjadala wetu kwamba, 'chimbuko la *Hip hop* ni sanaa za maonesho' tumeweza kuthibitisha kwa kupitia sifa au vigezo pambanuzi vya muziki wa *Hip hop* na kuviona jinsi vinavyojitokeza katika muziki huu. Muziki huu wa *Hip hop* una 'usanaa wa maonesho' ambao unajipambanua kupitia katika maudhui (wazo au dhamira), ploti (msuko wa matukio au kisa), wahusika, muziki, uteuzi wa lugha, na vionwa (vifaa na vitu vinavyomsaidia mhusika kutekeleza uhusika wake). Kwa maelezo hayo, tunathibitisha kuwa, chimbuko la *Hip hop* sio 'uasi' na wala sio 'uhuni' bali ni sanaa ya maonesho ambayo ilibuniwa ili kuelezea maisha ya wanajamii husika.

## Marejeleo


Banjoko, A. (2012 ). *A Response: Hip hop Is Indeed Black Culture.* www.daveyd.com/addissablackart.html

Brockett, O. (1964). *The Theatre: An Introduction*. United States of America: Holt, Rinehart, and Winston Inc.

Dambaya H, na J. Mbilinyi (Mr II) katika kipindi cha *Keki ya Taifa* kilichorushwa

hewani na Redio na TV Mlimani, Jumanne tarehe 31 Oktoba, 2011.

Mangesho, P. (2003). *Global Cultural Trends: The case of Hip – Hop Music in Dar esSalaam.* Unpublished MA Dissertation, University o of Dar es Salaam.

Matonya, *Dunia Mapito,* www.museke.com/node/2162 umepakuliwa Jumapili 6 Novemba, 2011.

Masonga, M. (2005). *The Dramatic Elements in Bongo Fleva Musical Video Performnces*: A case Study of *Starehe* (Ferooz), *Nitakufaje* (Crazy JK) and *Siamini* (TID). Unpublished MA Dissertation. University of Dar es Salaam.

Mlama na Balisidya, (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonesho.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Open University of Tanzania

Omari, S. (2009). *Tanzania Hip hop Poetry as Popular Literature.* Unpublished PhD Thesis, University o of Dar es Salaam

Perullo, A. (2003). *"The Life That I Live": Popular Music Agency and Urban Society in Dar es Salaam Tanzania.* Indiana University.

Rubanza, Yunus. I. (1994). *Fasihi Simulizi: Majigambo (Ebyebugo).* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Samwel, M. (2012). "Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva." (Haijachapishwa), Tasinifu ya Uzamivu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Semzaba, E. (1997). *Tamthiliya ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Open University of Tanzania

Z. Anton. *Binti Kiziwi.* www.museke.com/node/2162 umepakuliwa tarehe 6 Novemba, 2011